JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE
SHULE YA SEKONDARI ITIPINGI

S.L.P 600
MAKAMBAKO
Barua pepe …….
Mkuu wa Shule: 0755-706924
Makamu: 0710191115
Mwl. wa Taaluma; 0658395299
Tarehe: ……

Kumb.Na.ITSS/REG.NO.S.1094
Jina la mwanafunzi……
……
S.L.P ……
…….

YAY: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITIPINGI WILAYA YA NJOMBE MKOA WA NJOMBE MWAKA 2021

1.0. Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika shule hii mwaka 2021 Shue ya Sekondari ITIPINGI ipo umbali wa Kilometa 08 kutoka barabara kuu iendayo Njombe, Ukitokea Ilunda na kama kilometa 15 Ukitokea Mji wa Makambako, Usafiri wa Basi kutoka Mji wa Makambako unapatikana katika kituo cha Mabasi cha Makambako. Mhula wa kwanza wa Masomo utaanza Tar.11/01/2021.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

- WAVULANA: Shati mbili (2) nyeupe Mikono mifupi, Suruali moja ya Khaki na rangi ya damu ya mzee.
- WASICHANA: Sketi na suruali yake rangi ya damu ya mzee Pea 1, Sketi na suruali yake ya kijani jeshi pea 1, (Mashati 2 Meupe) Mikono mifupi.

A) Hijabu iwe ya rangi nyeupe

- Sweta 1 Rangi ya kijani jeshi
- Viatu vyeusi vya Ngozi na siyo yebo yebo
- Wasichana wavae soksi nyeupe
- Wavulana Soksi nyeusi
  NB: (Sketi mshono wa linda boksi)
- Track rangi ya bluu bahari kwa wote

B) Sare ya michezo kwa shule hii ni raba jozi moja kwa wote, bukta na tisheti rangi ya Dark blue.

2.2 Daftari (10) Counter quire (4) Kalamu na mkebe wa hesabu.

2.3 Matibabu na nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani ni jukumu la mzazi/ Mlezi.

2. 4 Nauli ya wanfunzi wa bweni kwenda na kurudi nyumbani wakati wa likizo, pia ni jukum la mzazi/ Mlezi

NB: Mahitaji haya yote yatakaguliwa mara tu mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu sabuni, Mswaki, Dawa ya meno, Taulo, Mafuta ya kupaka ni muhimu sana.

3.0 Sheria **na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule hii inaendeshwa kwa muhimu wa sheria ya Elimu Namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995.

Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshai wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mamboya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhuriao mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakatia wote wa uanafunzi wako katika shule.
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i. Kutunza mali za umma

3.1 Makosa **yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamaishwa shule.**

a. Wizi
b. Uasherati na Ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na Matumizi ya Madawa ya Kulevya kama uvutaji Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na Kadhalika.

e. Kupigana au Kupiga.
f. Kuharibu kwa Makusudi mali ya Umma
g. Kudharau Bendera ya Taifa.
h. Kuwa Mjamzito/ Kupata Mimba/ Kusababisha Mimba.
i. Kuoa au Kuolewa
j. Kutoa Mimba
k. Kugoma, Kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na Usalama wa Shule au Watu.
l. Kukataa adhabu kwa Makusudi.
m. Kuwa na Simu ya Mkononi

3.2 Mambo **mengine muhimu yanaopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na Mwanafunzi:-**

a. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni
b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makasa ya jinai.
c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheri, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d. Mwanafunzi aje na ufagio wa chelewa na jembe dogo/ Si lazima liwe jipya ni kwaajili ya usafi shuleni

3.3 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

3.4 Mahitaji ya Hosteli kwa Wavulana/ Wasichana

i. Godoro futi 2.5
ii. Blanketi zito 1
iii. Shuka 2 rangi ya pinki
iv. Vyombo vya Chakula, Vifaa vya usafi wa mwili, Mswaki, Kiwi, Taulo, Mafuta ya kupakaa n.k

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YETU

“Maisha ya shule ni mazuri sana kwa wale wanaofuata taratibu zilizowekwa”

……..

C.A. NKWITA
MKUU WA SHULE
0755-706924

FOMU YA KUKUBALI/KUKAKATAA MASOMO YA SEKONDARI

……
……
…….
TAR……..

MKUU WA SHULE,
ITIPINGI SEKONDARI,
S.L.P 600,
MAKAMBAKO.

YAH: KUKUBALI/KUKATAA NAFASI YA KIDATO CHA KWANZA
MWAKA 2021

Mimi…….....me/ke niliyesom shule ya msingi……..
Nimekubali/nimekataa nafasi nya kusoma Sekondari kwa sababu……..
……..
Kwa aliyekubali nafasi:
Baada ya majadiliano na wazazi wangu nitakuwa tayari kufuata taratibu na sheria za shule zote kwa hiari yangu.Naahidi kushirikianana wazazi /walezi .
Walimu na watumishiwengine kwa kutoleta usumbufu wa aina yoyote ile.

Jina la mwanafunzi……
Namba ya kufanyiaMtihani DRS la saba ni:……
Sahihi ya mwanafunzi……..

Jina la Mzazi/Mlezi……..
Sahihi ya Mzazi/Mlezi……
Namba ya simu……..

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI:

1. Una wazazi wote wawili NDIYO/HAPANA……
2. Mzazi mmojakama alifariki ni Mama/Baba……..
3. Ni yatima huna wazazi wote wawili……
   Ndiyo anakulea wewe ni nani wako?.....
4. Mzazi/Mlezi wako anafanya shughuli gani……..
   ……..

NB: JAZA VIPENGELE VYOTE KABLA HUJAFIKA SHULENI.

SHERIA NA KANUNI YA SHULE

Sheria na kanuni za shule zinalenga kumlea na kufanya mwanafunzi kuwa na maadili na makuzi yanayokubalika katika Taifa letu. Kanuni na sheria hizi ni kwa shule zote za Tanzania. Kukiuka Kanuni na sheria katika shule moja ni kosa katika shule zote nchini.Utii na nidhamu shuleni ni siri ya mafanikio.

ITIPINGI SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM FOR STUDENTS.

To be completed by a medical officer of the Government hospital in respect to all form one entrance.

Full name……
Age…….

1. Blood count (Red and White)……..
2. Stool examination……..
3. Urine Analysis…….
4. Syphilis test……
5. Eye test……
6. T.S. test……..
7. Ears…….
8. Chest……..
9. Abdomen……
10. Spleen…….

ADDITIONAL INFORMATION: Geophysical defect, Familydiseases etc.

……
……

I certify that the above students/pupil is FIT/NOT FIT to pursue studies in secondary level.

Signature:…….....designation…….
Date:…….station……

NOTE: Medical officer: thank you for the notification.

MWANAFUNZI: HAKIKISHA FOMU HII IMEJAZWA KATIKA HOSPITALI YA SERIKALI KABLA HUJAFIKA SHULENI.UNAPOKUJA UJE NAYO.

MUHIMU SANA

Mwanafunzi awapo katika shule hii hapaswi kujihusisha na masuala yoyote yale ya utovu wa nidhamu ikiwa ni pamoja na:-

- Kuharibu kwa makusudi miundombinu ya shule mfano:

a) Kuchoma moto majengo ya Serikali (Madarasa, Mabweni, Ofisi za Walimu)

b) Kuharibu viti, Meza au madawati ya shule

c) Kuchafua kuta za madarasa kwa kuchora, kuandika matusi, kuvunja vioo vya madirisha au kuharibu mali yoyote ya shule, Mzazi/ Mlezi utawajibika kulipa. Endapo utashindwa mwanao atafukuzwa shule mara moja.